Government of JERSEY

# Haki zako kama mfanyakazi anayefanya kazi Jersey

Jersey ni mahali pazuri pa kufanya kazi, na afya yako, usalama wako na haki zako za kisheria zote zinalindwa.

Kijitabu hiki kina taarifa kuhusu msaada na ushauri unaopatikana kwako, ikiwa una maswala.

Iwapo utawahi kufikiri kuwa unatendewa vibaya, zungumza na mwajiri wako kwa njia isiyo rasmi ili umwambie kilicho kibaya, na jinsi unavyofikiri kinaweza kuboreshwa.

Ikiwa mambo hayatakuwa bora zaidi, basi unaweza kuwasilisha malalamishi rasmi.

Kijitabu hiki kina maelezo ya mashirika ambayo yatakusaidia bila malipo, na bila kumjulisha mwajiri wako.

## Haki Zako

Kwa mujibu wa sheria, mwajiri wako ni lazima akupe:

- mkataba ulioandikwa ndani ya siku 28 baada ya kuanza kazi: bila kujali mkataba wako wa ajira, ni lazima upewe taarifa hii ya masharti ya awali ya ajira.
- angalau £10.50 kwa saa (Kiwango cha mwaka wa 2023 cha 'mshahara wa chini')
- risiti ya mshahara (karatasi zinazoonyesha ulicholipwa, na makato yoyote ya mwajiri wako, ikijumuisha kwa nini yamefanywa)
- mapumziko yasiyokatizwa ya
- dakika 20 kila siku ikiwa unafanya kazi kwa zaidi ya saa 6 kwa siku hiyo
- saa 24 katika kipindi chochote cha kufanya kazi kwa siku saba
- likizo inayolipiwa ya wiki 3 kwa mwaka mzima (kiasi hiki kitashuka ikiwa utafanya kazi kwa chini ya mwaka mmoja)
- nafasi nzuri ya kubadilisha masharti ya ajira yako ikiwa unahitaji

Ikiwa unalipwa kwa kiwango cha chini cha mshahara wa £10.50 kwa saa (kiwango cha mwaka wa 2023), na unapata malazi au chakula na kazi yako kama sehemu ya mkataba wako wa ajira, mwajiri wako anaweza kukutoza tu kiwango cha juu zaidi cha:

- £115.00 kwa wiki (kwa malazi tu)
- £153.28 kwa wiki (kwa chakula na malazi)

### Tem o direito de não ser despedido injustamente do seu emprego.

Iwapo umefanyia kazi mwajiri wako kwa zaidi ya wiki 52, ni lazima upewe sababu ya haki ya kufukuzwa kazini. Ikiwa bado hujafanya kazi kwa wiki 52, unaweza kudai kufukuzwa kazini kwa njia isiyo ya haki katika hali fulani, ikijumuisha:

- Ikiwa unalalamika kwamba mwajiri wako hajakupa mkataba ulioandikwa na anakufukuza kwa kuwasilisha lalamishi hili
- Ikiwa utajiunga na chama cha wafanyakazi na mwajiri wako akakufukuza kwa kufanya hivyo au kwa kushiriki katika shughuli za chama cha wafanyakazi

### Una haki ya kutotendewa tofauti kazini kwa sababu ya sifa hizi zinazolindwa:

- mbari (utaifa wako, rangi ya ngozi yako au kabila lako)
- umri
- jinsia (kiume, kike nk.)
- mwelekeo wa kijinsia (mashoga, wasagaji, nk.)
- ugawaji upya wa jinsia (mtu ambaye amebadilisha jinsia)
- ujauzito na hali ya kuwa mama
- ulemavu (kama wewe ni mtumiaji wa kiti cha magurudumu, mtu aliye na matatizo ya kupata masomo, nk.)

### Una haki ya kufanya kazi katika sehemu ambayo ni salama

Hutarajiwi kufanya kazi ikiwa mahali pako pa kazi sio salama. Ikiwa una maswala kwamba eneo lako la kazi huenda likawa sio salama, unaweza kuwasiliana na Ukaguzi wa Afya na Usalama (Health and Safety Inspectorate) kuptia 01534 447300 au **hsi@gov.je**

## Kufanya kazi ukiwa na notisi

Ni lazima uwe na muda wa chini wa kupokea notisi (wakati huo unaendelea kufanya kazi na kulipwa) ikiwa mwajiri wako anataka kukuachisha kazi:

Huduma ya afya huko Jersey

| Duração do contrato de trabalho | Período de pré-aviso |
|---|---|
| Inferior a 2 anos | Pré-aviso de 1 semana |
| 2-3 anos | Pré-aviso de 2 semanas |
| Superior a 3 anos | Pré-aviso extra de 1 semana por ano de serviço contínuo, até um máximo de 12 semanas |

Unaweza pia kuhitaji kutoa notisi kwa mwajiri wako ikiwa unakusudia kuacha kazi, kulingana na mkataba wako.

Ikiwa umefanyia kazi mwajiri wako kwa miaka miwili au zaidi, na ukapoteza kazi yako kwa sababu ya kupunguzwa kwa waajiriwa, una haki ya kupata malipo ya kupunguzwa kwa waajiriwa. Hii inatumika kwa wafanyakazi wote, bila kujali mkataba wa ajira walio nao. Malipo ya chini ya kisheria ya kupunguzwa kwa waajiriwa kazini ni malipo ya wiki kwa kila mwaka wa ajira.

## Huduma ya afya huko Jersey

### Ajali na Hali ya Dharura

Ikiwa unahitaji ambulensi, piga simu kwa 999 au 112.

Idara ya Hali Dharura ya Jersey iko kwenye Parade, St Helier na inafunguliwa saa 24 kwa siku, kila siku ya mwaka. Huduma ya dharura ni ya bila malipo, lakini unaweza kulipia huduma zingine za hospitali.

### Afya ya akili

Ikiwa una tatizo la afya ya akili, piga simu kwa 01534 445290.

Timu ya Kutathmini Tatizo la Afya ya Akili hailipishi na inapatikana saa 24 kwa siku, kila siku ya mwaka.

### Madaktari wa Kawaida na Famasia

Unaweza kupata orodha ya Madaktari kwenye Saraka ya Mtandaoni ya Jersey (Jersey Online Directory) (**www.jod.je**)

Huduma za Kawaida na famasia ni biashara za kibinafsi na huchagua ni kiasi gani watatoza kwa huduma zao. Muulize daktari wako kuhusu ada wanazotoza ili ujue gharama ya huduma na ada zozote za ziada (kama vile vipimo vya damu).

Baada ya kufanya kazi Jersey, na kulipa michango ya Hifadhi ya Jamii kwa miezi sita, una haki ya kupata ruzuku kutoka kwa Mfuko wa Bima ya Afya. Ruzuku inashughulikia watoto (chini ya miaka 16) katika nyumba pia, na inajumuisha:

- ada ya bei nafuu kwa mashauriano ya GP
- dawa za bila malipo zinazoagizwa na daktari
- chanjo ya bila malipo ya mafua kwa makundi yaliyo katika hatari kubwa
- uchunguzi wa mlango wa uzazi bila malipo (kipimo cha kupaka kwa wanawake na walio na uke na uume)

### Matibabu ya hospitali yasiyo ya dharura

Kwa hali zisizo za dharura, weka miadi na daktari wako.

Ikiwa daktari wako atakuelekeza kwa matibabu ya hospitali yasiyo ya dharura, unaweza kulipa, ingawa matibabu yasiyo ya dharura ni ya bila malipo kwa wafanyakazi ambao wamekuwa wakifanya kazi huko Jersey kwa:

- miezi 6 kabla tu ya kutafuta matibabu au
- angalau miezi 6 mfululizo wakati wowote ndani ya miaka 3 iliyopita.
- Hii inashughulikia watoto wao (chini ya miaka 18) na wanandoa wao pia.

Serikali pia inatoa matibabu yasiyo ya dharura bila malipo kwa wafanyakazi ambao wana hadhi ya walio na 'leseni' tangu siku wanayoanza kazi.

## Kuendesha gari ukiwa Jersey

Ni lazima upate leseni ya kuendesha gari iliyotolewa na Jersey ikiwa unafanya kazi huko Jersey kwa miezi 12 au zaidi na upange kuendesha gari katika Kisiwa hicho.

Leseni za kuendesha gari kutoka nchi zingine ni halali, na zinaweza kubadilishwa na kupata leseni ya Jersey, lakini sivyo ilivyo kwa leseni zote. Unapaswa kuwasiliana na:

- ukumbi wa parokia katika parokia unayoishi (nenda kwenye **www.comite.je** kwa maelezo zaidi)
- Viwango vya Dereva na Gari (Driver and Vehicle Standards) (**gotogov.je** tafuta DVS)

## Maswali yanayoulizwa mara kwa mara

*S. Ninatumia kibali cha kazi ambacho muda wake bado haujakwisha lakini uhusiano wangu na mwajiri wangu umevunjika kabisa. Je, ninaweza kubadilisha waajiri bila kuondoka kisiwani?*

J. Chini ya sera ya kibali cha kazi cha Jersey huwezi kubadilisha na kupata mwajiri mwingine isipokuwa uwe umekamilisha kipindi cha miezi 12 cha ajira na mwajiri wako uliye naye sasa. Katika hali za kipekee unaweza kubadilisha mwajiri pale ambapo kuna sababu zinazolazimisha kufanya hivyo.

*S. Je, ninaweza kufanya nini ikiwa mwajiri wangu ana pasipoti yangu na anakataa kuirejesha?*

J. Hakuna msingi wa kisheria kwa mwajiri wako kubakia na pasipoti yako. Ikiwa una wasiwasi, unapaswa kutafuta ushauri kutoka kwa Citizens Advice. Unapaswa pia kuwasiliana na Idara ya Uhamiaji ikiwa mwajiri wako atabakia na pasipoti yako na anakataa kuirejesha – **immigration@gov.je**

*S. Je, mwajiri wangu anaweza kuchukua pesa ngapi kwa kusafiri kwenda na/au kutoka Jersey?*

J. Ni juu yako kukubaliana na mwajiri wako kuhusu gharama za kusafiri kwenda na kutoka Jersey. Unapaswa kukubaliana hili kwa maandishi pamoja na mwajiri wako mtarajiwa kabla ya kukata tiketi au kusafiri kwenda Jersey.

*S. Je, vikomo vya muda ni vipi vya kutoa dai kwa Mahakama ya Ajira na Ubaguzi (Employment & Discrimination Tribunal)?*

J. Madai mengi (ikijumuisha kuachishwa kazi kwa njia isiyo ya haki na ubaguzi) yanapaswa kupokelewa na Mahakama ndani ya wiki 8 kuanzia tarehe ambayo ajira yako iliisha au tukio ambalo unalalamikia lilitokea. Unaweza kupata taarifa zaidi kutoka kwa Mahakama – maelezo ya mawasiliano yameonyeshwa hapa chini.

## Maelezo ya mawasiliano

Ikiwa una wasiwasi kuhusu kipengele chochote cha ajira yako, unaweza kupata msaada na ushauri kutoka kwa mashirika kadhaa.

Hakuna shirika lolote kati ya haya litakalowasiliana na mwajiri wako au mamlaka bila idhini yako.

Wao wataweka hoja yako kwa usiri.

Ushauri watakaokupa hautalipishwa.

**Jersey Advisory & Conciliation Service**
3rd Floor, 1 Seale Street, St Helier,
Jersey JE2 3QG
01534 730503
**www.jacs.org.je**

**Citizens Advice Jersey**
St Paul's Centre, New Street, St Helier,
Jersey JE2 3PW
01534 724942
**www.citizensadvice.je/category/employment**

**Friends of Africa**
www.foajersey.org.je

**Trade Union representative**
Unite the Union, 7D Spectrum, Gloucester Street,
St Helier, Jersey, JE2 3DA
01534 872584 or **Jersey@unitetheunion.org**

**Jersey Employment and Discrimination Tribunal**
1st Floor, International House, 41 The Parade,
St Helier, Jersey JE2 3QQ
01534 441380
**registrartribunalservice@courts.je**

**Jersey Customs and Immigration Service (JCIS)**
01534 448000
**immigration@gov.je**

**Customer and Local Services (CLS)**
01534 444444
**customerservice@gov.je**

**Honorary Consulate of Portugal**
Burlington House, St Saviour's Road, St Helier,
Jersey JE2 4LA
01534 877188
**consuladoportugaljersey@hotmail.com**

**Jersey International Cultural Centre**
Jersey Library, Halkette Place, St Helier,
Jersey, JE2 4WH
01534 448713
**icc@gov.je**